**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**
**HALMASHAURI YA WILAYA BUKOBA**
***Shule ya Sekondari Nyakato, S.L.P 6, Bukoba.***

Namba za simu:
Mkuu wa Shule: *0754772580/ 0785750630/ 0621909813*
Makamu Mkuu wa Shule: *0621011331/0758133998*
Barua pepe: ***secondarynyakato@gmail.com***

*Tar. 30/03/2022*

Mzazi/Mlezi wa…………………………………

S.L.P…………………………………………...

………………………………………………

**YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI NYAKATO HALMASHAURI YA WILAYA BUKOBA MKOA WA KAGERA MWAKA 2022.</u>**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano katika shule hii mwaka 2022 kwa Tahasusi ya…………Shule ya Sekondari Nyakato ipo umbali wa Kilometa 6 Kusini mwa Manispaa ya Bukoba. Usafiri wa pikipiki kutoka mjini kufika shuleni si zaidi ya **Tshs. 2,000**.

Muhula wa masomo utaanza **Septemba, 2022.** Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe**…….**na mwisho wa kuripoti ni tarehe**…….**

## 1. ADA NA MICHANGO

Mchanganuo ufuatao ni wa malipo ya ada na michango itakayolipwa.

1. (a) **ADA**

| S/N | MALIPO | KIASI |
|---|---|---|
| | Ada | 70,000/= kwa mwaka au 35,000/= kwa muhula. |

### (b) MICHANGO MINGINE

| S/N | MALIPO | KIASI |
|---|---|---|
| 1. | Tahadhari | 5,000/= inalipwa mara moja na **haitarejeshwa** |
| 2. | Taaluma | 20,000/= kwa mwaka |
| 3. | Walinzi, wapishi na wafanyakazi wengine | 30,000/= kwa mwaka |
| 4. | Huduma ya kwanza | 10,000/= kwa mwaka |
| 5. | Kitambulisho na picha | 6,000/= inalipwa mara moja |
| 6. | Nembo ya shule | 2,000/= mara moja |
| 7. | Ukarabati wa Samani | 15,000/= kwa mwaka |
| 8. | Mtihani wa utimilifu (Mock) | 20,000/= mara moja |

Malipo ya ada na michango mingine ambayo jumla yake ni **Tsh. 178,000/=** ilipwe katika akaunti ya shule namba **31801100049** yenye jina **Nyakato Secondary School Recurrent Account** ya Benki ya **NMB**

Ni lazima mwanafunzi afike shuleni na stakabadhi ya malipo (Bank pay- in-slip) ambayo itawasilishwa kwa mhasibu wa Shule na mzazi atapewa risiti. Andika majina sahihi ya mwanafunzi na tahasusi atakayosoma katika stakabadhi ya malipo.

## 2. SARE NA MAHITAJI MENGINE

Mwanafunzi anatakiwa afike shuleni akiwa na sare na mahitaji mengine kama ilivyoainishwa hapa chini.

| S/N | AINA YA SARE/ MAHITAJI MENGINE |
|---|---|
| 1. | Mashati mawili meupe ya mikono mifupi |
| 2. | Suruali tatu( mbili rangi **nyeusi** na moja rangi ya **kahawia** iliyoiva) zinazofunika soksi zenye upana usiopungua **sentimeta 18** chini. |
| 3. | Viatu vyeusi jozi mbili vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi |
| 4. | Soksi nyeusi jozi mbili |
| 5. | T-shirt 2 za rangi ya **NJANO** iliyoiva zenye kola na zisizo na maandishi ( Unaweza kuipata shuleni kwa Tsh.15,000/= kila moja) |
| 6. | Sweta moja ya rangi ya **MAROON** (Unaweza kuipata shuleni kwa Tsh.15,000/=) |
| 7. | Bukta moja ya rangi ya bluu yenye michirizi myeupe |
| 8. | Raba za michezo |
| 9. | Track suit rangi ya **KIJANI** iliyoiva yenye michirizi myeupe isiyo na maandishi yoyote. |
| 10. | Godoro moja futi $2\frac{1}{2}$ kwa inch 3 |
| 11. | Mashuka mawili ya rangi ya pinki na blanketi moja |
| 12. | Mto na foronya moja yenye rangi ya pinki |
| 13. | Chandarua moja |
| 14. | Ndoo moja ya lita 10 (kwa matumizi binafsi) |
| 15. | Taulo , malapa, sabuni za kutosha, mswaki na dawa ya meno |
| 16. | Sahani, Bakuli, kikombe nusu lita na kijiko |
| 17. | "Toilet papers" za kutosha |
| 18. | Mwavuli |
| 19. | Sanduku moja imara |
| 20. | "Rain Boot" Viatu vya mvua |
| 21. | "Dissecting Kit" kwa wanafunzi wa masomo ya elimu viumbe (Biology) |
| 22. | Vitabu vya masomo ya tahasusi husika **(orodha ya vitabu pendekezwa imeambatishwa)** |
| 23. | Taa ya sola au betri. **( Isiwe ya kuchaji kwenye umeme)** |

*ANGALIZO:*

Nguo nyingine zozote haziruhusiwi kabisa shuleni. Mwanafunzi atakayeripoti na nguo ambazo hazikuainishwa katika fomu hii **atalazimika kuzirudisha nyumbani**.


## 3. MAHITAJI MENGINE YA KITAALUMA:

1. Nakala ya matokeo ya kidato cha nne (result slip).
2. Nakala ya cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate).
3. Mkebe wa Hisabati (Mathematical set) na scientific calculator aina ya CASIO Fx-991MS( kwa tahasusi za Sayansi na Jiografia, unaweza kuipata shuleni kwa Tsh. 40,000/=).
4. Begi la kubebea vitabu na madaftari.
5. Counter books kumi (Quire three) kwa ajili ya masomo darasani.
6. Madaftari madogo 10 kwa ajili ya mazoezi ya kila siku darasani.
7. Kalamu za wino, rula na penseli za kutosha.
8. Ream 1 ya karatasi aina ya A4 isiyo na mistari (kwa muhula).
9. Graph pad 1 yenye kurasa 50 (kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi na jiografia).
10. Box file moja kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu binafsi za mwanafunzi.

## 4. VIFAA VYA USAFI

Ili kuwafundisha na kuwajengea wanafunzi wetu tabia ya usafi na utunzaji wa mazingira na pia kuweka shule yetu katika hali ya usafi na mazingira ya kuvutia, mwanafunzi afike shuleni akiwa na vifaa kama inavyooneshwa hapa chini;

| S/N | AINA YA KIFAA | TAHASUSI |
|---|---|---|
| 1. | Kotama | HKL, PCB & CBG |
| 2. | Squizer | WOTE |
| 3. | Mfagio 1 laini wa plastiki (soft broom) | CBG, PCM & PGM |
| 4. | Mfagio 1 wa nje (chelewa) - mfano wake angalia chini ya jedwali | WOTE |
| 5. | Ndoo kubwa ya lita 20 | PCB,PCM & PGM |
| 6. | Reki | HGE |
| 7. | Brush ya chooni | WOTE |
| 8. | Panga lililonolewa | HGK |
| 9. | Seti ya ndoo ya kudekia | WOTE |
| 10. | Fyekeo iliyonolewa | HKL,HGK & HGE |



## 5. BIMA YA AFYA

Kila mwanafunzi afike shuleni na Taslimu TSH. 5000/= kwa ajili ya bima ya afya **ILIYOBORESHWA** (CHF) ambayo italipwa kila mwaka. Mwanafunzi mwenye kadi ya bima ya NHIF mwenye umri usiozidi miaka 21 hatahusika na mchango huu, na afike na kadi hiyo.

## 6. VIAMBATISHO

Hakikisha unasoma na kujaza viambatisho vifuatavyo:-

- Fomu ya kupima afya ya mwanafunzi.
- Fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi.
- Sheria za shule.
- Fomu ya kukubali nafasi.

## 7. SIKU YA KURIPOTI SHULENI

- Kila mwanafunzi aje amevaa **sare ya shule** iliyoainishwa kwenye fomu hii.
- Siku za kuripoti ni Jumatatu hadi Ijumaa kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 9.30 mchana.

Mwisho, napenda kumkaribisha mwanao katika Shule ya Sekondari ya Nyakato, mahali ambapo tunatoa elimu na malezi bora kwa vijana ambao ni nguvu kazi yaTaifa letu la Tanzania kwa siku zijazo. Mwanafunzi ajiandae kwa moyo na ari ya kutaka kuelekezwa, kufundishwa na kujifunza. Nidhamu, utii, heshima, uwajibikaji na kujituma ni mambo muhimu na ya msingi sana yanayotiliwa mkazo na kusisitizwa katika Shule yetu wakati wote.

Nakutakia mafanikio mema na karibu sana katika Shule ya Sekondari ya Nyakato.

…………
RWELAMILA D.D
**MKUU WA SHULE**

HEAD OF SCHOOL
NYAKATO SEC. SCHOOL
3 0 MAR 2022
P.O.Box 6 BUKOBA
KAGERA

# *KIAMBATISHO A*
# *SHERIA ZA SHULE*

Sheria, taratibu na kanuni hizi zifuatwe na kila mwanafunzi bila kusita na kwa wakati wote awapo shuleni. Kukiukwa kwa sheria, taratibu na kanuni hizi kutamsababisha mwanafunzi kupewa adhabu kali ikiwemo kurudishwa nyumbani.

(i) Mwanafunzi avae sare za shule wakati wote wa siku za masomo na siku za ibada. Baada ya masomo na siku za Jumamosi na Jumapili atavaa mavazi yaliyoainishwa.

(ii) Mwanafunzi hataruhusiwa kuvaa kandambili au viatu vya aina nyingine wakati akiwa katika sare rasmi ya shule tofauti na viatu alivyoagizwa.

(iii) Mwanafunzi hatarusiwa kutoka nje ya shule bila ruhusa iliyoidhinishwa

(iv) Ni marufuku kabisa mwanafunzi kuingia kwenye nyumba ya mtumishi yeyote kwa sababu yoyote ile mchana au usiku, isipokuwa kwa kibali cha mwalimu wa zamu.

(v) Ikiwa mwanafunzi ana matatizo ya kinidhamu, kifamilia au ugonjwa ni mzazi/mlezi pekee ambaye picha yake ipo katika maelezo ya mwanafunzi atakayewajibika kufika shuleni kumchukua, kusikiliza, na kujadiliana na walimu kuhusu nidhamu au ugonjwa wa mwanaye. Mtu mwingine yeyote yule hatakabidhiwa wala kujadili matatizo ya mtoto asiye wake.

(vi) Kila mwanafunzi anatakiwa kulala katika kitanda na bweni alilopangiwa muda wote awapo shuleni.

(vii) Mwanafunzi kuhama bweni na kulala wawili ni kosa kubwa na ataadhibiwa vikali akibainika.

(viii) Vyakula na milo yote iliwe katika bwalo la chakula na vifaa vya chakula vitunzwe vizuri bwaloni.

(ix) Kila mwanafunzi anatakiwa kupata mlo wake katika meza yake aliyopangiwa na atawajibika kuisafisha kila mlo kwa utaratibu waliojiwekea.

(x) Jikoni ni mahali pa kutengeneza chakula, hivyo panatakiwa kuwa safi wakati wote. Wanafunzi hawaruhusiwi kuingia jikoni bila sababu ya msingi.

(xi) Vifaa vyote vya umeme kama vile redio, pasi na kamera nk. havirusiwi kwa mwanafunzi anapokuwa shuleni.

(xii) Mwanafunzi atakayelazimika kulala kwa ajili ya ugonjwa ni lazima apate kibali cha muuguzi wa shule.

(xiii) Mwanafunzi atakayeugua akiwa darasani na kuhitaji kupata matibabu katika zahanati ya shule anatakiwa kupata kibali kutoka kwa mwalimu wa zamu.

(xiv) Wageni hawaruhusiwi kuonana na wanafunzi wakati wa masomo. Mzazi atakayehitaji kutoa mahitaji yoyote kwa mwanaye atapokelewa na mwalimu wa zamu ambaye atayawasilisha kwa mwanafunzi kwa utaratibu maalumu uliopangwa. Kuwaona wanafunzi ni Jumamosi ya mwisho wa mwezi na si vinginevyo.

(xv) Mwanafunzi atakayeripoti shuleni baada ya saa kumi na mbili jioni wakati wa kufungua shule au apewapo ruhusa ya kwenda nje ya shule kwa sababu yoyote ile

**ATARUDISHWA NYUMBANI** na atalazimika kufika shuleni na mzazi/mlezi kwa ajili ya kutoa maelezo na sababu za kuchelewa kuripoti shuleni, hatua zaidi zitachukuliwa iwapo maelezo ya mzazi/mlezi hayataridhisha.

(xvi) Uharibifu wa mali za shule/umma wa aina yoyote ile mhusika au kundi husika, watagharimia urejeshwaji wa mali/samani/miundo mbinu kwa gharama zake/zao.

**MAKOSA YATAKAYOMSABABISHA MWANAFUNZI AFUKUZWE SHULE MARA MOJA**

(i) Wizi wa mali ya shule au ya mwanafuzi mwenzake.

(ii) Kuingia na **SIMU** shuleni au kukutwa na kadi, betri na chaja ya **simu**. Hakuna mwanafunzi atakayetunziwa simu shuleni.

(iii) Uasherati na uzinzi nje na ndani ya shule.

(iv) Ulevi wa pombe au madawa ya kulevya.

(v) Kuingia mahali panapouzwa kileo/pombe.

(vi) Kuvuta sigara, kutafuna mirungi na kuvuta ugoro.

(vii) Kutoa lugha ya matusi hadharani au kwa kificho kwa walimu na wanafunzi wenzake.

(viii) Kupigana hadharani au kutishia kumpiga mwanafunzi mwingine kwa sababu yoyote ile.

(ix) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma, miundombinu ya shule au mali za wanafunzi wenzake.

(x) Utoro kuanzia siku moja na kuendelea, mwanafunzi kulala nje ya shule baada ya kupewa ruhusa ya kutwa.

(xi) Kuchochea au kushiriki katika mgomo wowote au mikutano isiyo rasmi.

(xii) Kugomea adhabu halali iliyotolewa na viongozi wa baraza la wanafunzi, kiongozi wa darasa, mwalimu au mtumishi yoyote mwenye mamlaka.

(xiii) Kutohudhuria masomo darasani kwa muda wa siku 90 mfululizo.

Kila mzazi asome kwa makini sheria na taratibu hizi akiwa na mwanaye na ahakikishe amemsaidia mwanaye kuzielewa kwa ajili ya kuzifuata kwa makini. Baada ya kuzielewa, mzazi na mwanafunzi wasaini kukubaliana nazo pamoja na adhabu zinazoambatana nazo. Mzazi na mwanafunzi wasaini nakala tatu (3) za sheria hizi, nakala moja ibaki na mzazi, nakala halisi irudishwe shuleni na nakala moja ibaki na mwanafunzi kwa ajili ya kujikumbusha kila siku.

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi ……………………………….mzazi/mlezi wa ……………………….nimezisoma sheria za shule nikiwa na mwanangu na kujadili pamoja naye na amezielewa. Ninakubaliana kushirikiana na uongozi wa Shule katika malezi ya mwanangu na nitakubaliana na adhabu yoyote itakayoamuliwa na uongozi wa Shule pale mwanangu atakapokiuka mojawapo ya sheria na kanuni hizi.

Saini ya Mzazi/Mlezi…………………………………….Tarehe ……………………………

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi……………………………..wa kidato cha........nimesoma kwa makini sheria na taratibu za Shule nikiwa na mzazi/mlezi wangu. Nimejadiliana naye na nimezielewa vizuri kabisa. Ninaahidi kuwa nitazifuata, naendapo nitakiuka mojawapo ya sheria na taratibu hizi hatua zichukuliwe dhidi yangu. Ewe mwenyezi Mungu nisaidie.

Saini ya mwanafunzi………………………………… Tarehe………………………

Ni imani yangu kuwa utafuata taratibu hizi ili uweze kujifunza kwa bidii na kwa mafanikio yaliyo bora. Nakutakia kila la heri na karibu sana Nyakato Sekondari.

……….

RWELAMILA D.D

**MKUU WA SHULE**

HEAD OF SCHOOL
NYAKATO SEC. SCHOOL
3 0 MAR 2022
P.O.Box 6 BUKOBA
KAGERA

***KIAMBATISHO B***

***Shule ya Sekondari Nyakato***

*S.L.P 6, Bukoba. Simu: 0785750630/ 0621909813/ 0627023892*

Barua pepe: ***secondarynyakato@gmail.com***

## MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina la Mwanafunzi ................................. ...........................................
2. Tarehe ya kuzaliwa.................... ..................................................
3. Mahali alipozaliwa: Mkoa ........................... Wilaya ..................................
   Tarafa .............................. Kata ............. Kijiji /Mtaa ...........................
4. Dini .....................................Dhehebu ................................................
5. Jina la baba mzazi/mlezi..............................................................................
   Anuani ................................Namba ya simu......................................
   Kazi ya baba mzazi/mlezi .......................................
   Yuko hai?Ndiyo /Hapana (kata isiyohusika)
6. Jina la mama mzazi/mlezi............................................................ Anuani ....................................Namba ya simu.................................... Kaziya mama mzazi/mlezi .......................................
   Yuko hai?Ndiyo /Hapana (kata isiyohusika)

| *Picha ya baba mzazi/mlezi* | *Picha ya mama mzazi/mlezi* |
|---|---|

7. Ndugu wa karibu aliyeidhinishwa na mzazi/mlezi anayeweza kupewa taarifa za matatizo ya mwanafunzi kwa haraka endapo mzazi/mlezi hatapatikana.

   Jina kamili ............................................... Anuani ..............................
   Namba ya simu ............................................................
   Kazi yake .................................... Uhusiano na mwanafunzi ..................

| *Picha ya ndugu wa karibu* |
|---|

**KIAMBATISHO C**
**MEDICAL EXAMINATION FORM**

NAME OF STUDENT.................................................................................

To medical officer I/C of

.......................................... ........District/Regional/Referral/Designated Hospital,
P.O. BOX..........................................

Please examine the above named in full as to his physical and mental fitness for being able to pursue two years of Secondary School Education. In case of an acute Defect/disability in each category or subcategory may render the applicant ineligible of admission or eligible of admission to schools of students with special needs:-

(i) Blood pressure..........................................................................................

(ii) Sickle cell test..........................................................................................

(iii) (a) Eyesight..........................................................................................

(b) Hearing ..........................................................................................

(c) Spleen ..........................................................................................

(d) Venereal diseases..........................................................................................

(e) Leprosy ..........................................................................................

(f) Epilepsy ..........................................................................................

(h) Typhoid ..........................................................................................

(iv) Neuroses ..........................................................................................

(v) Other serious diseases ..........................................................................................

General comment(s) ..........................................................................................

Name ..........................................................................................
Designation ..........................................................................................
Official stamp .......................................... Date ................................

ANGALIZO: Mzazi athibitishe kuwa vipimo hivi vimefanyika kikamilifu na sio kujaza jina na saini ya mganga. Atakayegundulika shuleni kuwa hakuchukua vipimo kihalali atarudishwa nyumbani.

**KIAMBATISHO D**

***Shule ya Sekondari Nyakato***
*S.L.P 6, Bukoba. Simu:0785750630/ 0621909813/ 0627023892*
Barua pepe: ***secondarynyakato@gmail.com***


**FOMU YA KUKUBALI NAFASI**

Mimi ……………………………………nakubali nafasi ya kidato cha tano niliyopewa katika Shule ya Sekondari Nyakato. Ninaahidi kutii na kufuata kwa uaminifu sheria na taratibu zote za Shule, kujifunza kwa bidii, juhudi na maarifa kwa uwezo wangu wote ili kutimiza lengo la kufaulu kwa kiwango cha juu kwa faida yangu, familia yangu na Taifa kwa ujumla. Ninaahidi kuripoti shuleni siku iliyopangwa bila kuchelewa.

Saini ya mwanafunzi……………………..

Tarehe……………………………………

**KIAMBATISHO E – RANGI YA KAHAWIA**



## ORODHA YA VITABU VYA ZIADA NA KIADA VINAVYOPENDEKEZWA

Ili mwanafunzi aweze kupata elimu bora na yenye kumwezesha kukabiliana na mazingira halisi ya maisha anapaswa kuwa na vitabu. Ifuatayo ni orodha pendekezwa

### 1. KISWAHILI

- Vuta N`kuvute – Shafi Adam Shafi
- Mfadhili - Hussein Tuwa
- Usiku Utakapokwisha- Mbunda Msokile
- Kufikirika – Shaaban Robert
- Kwenye Ukingo wa Thim –Ebrahim Hussein
- Morani – Emmanuel Mbogo
- Kivuli Kinaishi –Said Mohamed
- Nguzo mama –Penina Mhando
- Kimbunga – Haji Gora Haji
- Mapenzi Bora – Shaaban Robert
- Fungate ya Uhuru – Mohamed S. Khatibu

### 2. CHEMISTRY

- Chemistry part 1, Text book for class XI (S.Chands)
- Chemistry part 1, text book for class XII (S.Chands)
- Advanced Chemistry 1 review (problems and solutions)
- Advanced Chemistry 2 review (problem and solutions)
- Chemistry for A' level (fourth edition) by RAMSDEN
- Conceptual Chemistry class XI by S. Chand
- Conceptual Chemistry class XII by S. Chand

### 3. BIOLOGY

- Advanced Biology for Secondary Schools –(Michael R.)
- Verma P.S and Pandey P.B (2010) S. Chands for class XI
- Cell structure and Organization – L. Msaki
- Taylor el al (2006), Biological science, third edition, Cambridge University Press.
- Glenn and Toole S. (1999), Understanding Biology for Advanced level, Fourth edition, Stanlet Thornes Publishers limited
- Verma P.S and Pandey P.B (2006) S. Chands for class XI, First edition, India, S. Chands and Company Limited.
- The (2019), Biology for Advanced Level Secondary Schools students Book form five and six.

## 4. ADVANCED MATHEMATICS

- Pure Mathematics 1&2- Backhouse
- Advanced Level Mathematics- C.J. TRANTER
- Mathematics for A level ( volume 1&2) – S . Chands
- Advanced Level Mathematics (vol 1)- L.K. Shayo

## 5. HISTORY

- Mastering Advanced Level History book I &II – Kato 2010
- Basic Themes in European Advanced Level History I &II – Ismail Ngobi-2012
- Major Events in African History paper I – Fr. Jovitus F. Kamala
- Towards Rural Development of Tanzania – By C.K Omary
- Ujamaa – Essay on socialism – By J.K Nyerere
- How Europe underdeveloped Africa – By Wolter Rodney
- A history of East Africa – By E.S Atieno Odhiambo, T.I.Ouso & J.F.M Williams
- A history of Africa (Volume 1) – By Assa Okoth
- A history of Africa (Volume 2) – By Assa Okoth
- Basic themes in Advanced level History , Paper 1& 2 – By F.M Mavunde
- Advanced level History, Paper 1& 2 – By Zisti Kamili
- Contemporary Historical Events, Paper 1& 2 – By Mwl. Shibitali C.K Tumaini

## 6. ENGLISH LANGUAGE

- Oxford Advanced Learner's Dictionary (12th Edition)

## 7. GEOGRAPHY

- General geography in diagrams – R.E Bunnett
- Practical geography for Africa – John M. Pritchard
- Physical geography for Africa - D. T Msabila
- Human and Economic geograph – D.T Msabila

## 8. PHYSICS

- S. Chand's Principals of Pysics for class XI &XIl
- Principle of Physics – Rogers Municaster
- Advanced Level Physics – Nelkon &Parlker
- Principles of Physics – Tom Duncan
- A – level Physics – Roge Muncaster (4th Edition)
- Comprehensive Physics (Volume 1 )
- Comprehensive Physics (Volume 2 )

**9. ECONOMICS**


- Economics Alive – Kamili Zisti (2010), Dar es salaam Kamili and general Book Supplier.
- Ambilikile, CM (2009). Economics for Advanced level paper 1 & 2
- Tayebwa, B (2011). Basic Economics 5th ed, Uganda: Genuine Publisher
- Odhiambo, A. Essentials for A level Economics paper 1& 2
- Ahuja, H.L (1970). Advanced Economic Theory: Microeconomic Analysis, Deth: S. Chand Publishing.
- Gupta, B.L (1990). Introductory to economic Theory, India: Arya Book Depot.


**10. GENERAL STUDIES**


- General Studies for Advanced Level Certificate (2011) , Form Five – Richard R. F. Mbalase
- General Studies for Advanced Level Certificate (2011) , Form Six – Richard R. F. Mbalase
- Bigirwa Mungu J. Understanding General Studies for Advanced Level 4th Edition.
- Nyambari Nyangwine (2010) General Studies notes form 5& 6 Nyambari Nyangwine Publisher.